# STD 4 END TERM 2 EXAM 2019

## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 dakika 40**

*Jaza pengo kwa kuchagua jibu sahihi katika swali la* **1 - 15.**

Mwaka ____1____ nitajiunga na darasa la tano. Masomo ____2____ darasa la nne yamenionyesha kuwa ____3____ kazi nyingi kule madarasa ya ____4____ kwa hivyo nimeamua kusonga ____5____. Tukifungua muhula wa ____6____ tutajiunga na ____7____ ambao pia watapanda ngazi. Ninajua kuwa kutakuwa na ____8____ nyingi. Hata hivyo nitajikaza katika ____9____ yote ili nipate ____10____ nzuri katika mtihani wa mwisho wa mwaka.

**1.** A. ujao B. uliopita C. ukifika D. utakaopita
**2.** A. wa B. ya C. za D. la
**3.** A. wana B. zina C. jana D. kuna
**4.** A. leo B. chini C. juu D. mbali
**5.** A. nyuma B. mbele C. mbali D. hapa
**6.** A. sasa B. watatu C. pili D. kwanza
**7.** A. wengine B. zingine C. yengine D. mengine
**8.** A. daftari B. kalamu C. kazi D. nguo
**9.** A. masomo B. bidii ile C. kuona D. kucheza
**10.** A. starehe B. chakula C. alama D. ujinga

Upishi ____11____ ni ule ambao umefanywa kwa uangalifu. Wapishi ____12____ hawazingatii ujuzi ____13____. Wao hupika chakula mradi kiive. Chakula hicho huwa ____14____. Watu hukionja na kukiacha. ____15____ yanayowachwa hupewa wanyama. Hawajui tofauti ya chakula bora na bora chakula.

**11.** A. kizuri B. mzuri C. zuri D. nzuri
**12.** A. mengi B. wingi C. wengi D. nyingi
**13.** A. wowote B. yoyote C. chochote D. kokote
**14.** A. mbaya B. mabaya C. mbaya D. kibaya
**15.** A. Masalia B. Maporo C. Uporo D. Mwiku

*Jibu maswali kuanzia 16 hadi 30 kufuatia maagizo uliyopewa.*

**16.** Andika tarakimu hii kwa maneno: 1.010.
A. Elfu kumi na kumi.
B. Elfu moja na kumi.
C. Elfu moja na kumi elfu.
D. Moja sufuri na kumi.

**17.** Babu yangu huniita ________.
A. binamu
B. mjomba
C. mjukuu
D. shemeji

**18.** Kamilisha methali ifuatayo
Teke la kuku halimwumizi ________.
A. mwewe
B. mtu
C. mwenyewe
D. mwanawe

**19.** Fatuma mchafu ni ________.
A. istiara
B. tashbihi
C. kitendawili
D. kivumishi

**20.** Kanusha sentensi:
Nimekula chakula chako.
A. Sijala chakula chako.
B. Twala vyakula vyako.
C. Nala chakula chako.
D. Sili chakula chako.

**21.** Kamilisha sentensi:
Shati langu ________ limechafuka.
A. leupe
B. nyeupe
C. cheupe
D. jeupe

**22.** Andika kwa wingi.
Yeye amesoma
A. Wao wamesoma
B. Wao hawajasoma
C. Sisi tumesoma
D. Nyinyi mmesoma

**23.** Ni mnyama gani mwenye tamaa nyingi?
A. panya
B. fisi
C. sungura
D. paka

**24.** Daktari alimdunga mgonjwa ________.
A. shindano
B. mashindano
C. sindano
D. shidano

**25.** Tafadhali mwalimu niende ________.
A. msalani
B. masalani
C. kukojoa
D. kwa darasa

**26.** Anayeendesha ndege huitwa ________.
A. tarriboi
B. kadawala
C. dereva
D. rubani

**27.** Taja jina la umbo hili



A. zigzagi
B. mstari sambamba
C. mstari mkunjufu
D. mraba

**28.** Rangi ya damu ni ________.
A. kijani kibichi
B. zambarau
C. nyekundu
D. nyeusi

**29.** Nyumba ya ng'ombe ni zizi, nayo nyumba ya konokono ni ________.
A. gamba
B. kizimba
C. kiota
D. kombe

**30.** Kinyume cha tajiri ni ________.
A. maskani
B. maskini
C. masikini
D. mpotevu

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 31 – 40*

Ni jambo la kuhuzunisha mno tunapowasikia madereva wengi na abiria wakilalamikia usalama wao barabarani na hasa nyakati za usiku.

Serikali haionekani kukisikiza kilio chao. Ndiposa nauliza, ni lini tutakuwa na usalama katika barabara zetu hapa nchini Kenya?

Majuzi tulisikia madereva wanaotumia barabara kuu ya Nairobi-Nakuru wakilalamika kuhusu ukosefu wa usalama wao na hiyo haikuwa mara ya kwanza kwao. Sehemu ya Salgaa imegonga vyombo vya habari kama mhali hatari ambapo ajali hutokea mara kwa mara na pia madereva wanaposafirisha bidhaa hushambuliwa mara nyingi.

Bidhaa hizo hupatikana katika masoko ya Nakuru, Mogotio, Molo, Naivasha, Gilgil na miji mingi mingineo. Wananchi hununua madukani hayo bila kujua ni bidhaa za wizi.

Kwa kweli mimi nawasihi tu wananchi watokao sehemu hizo wasitumie fursa hii kujinufaisha bali wasaidiane kukabiliana na kupambana na makundi hayo yanayowatatiza madereva hasa katika sehemu ya pinde za barabara na milimani.

**31.** Kilio cha madereva na abiria ni?
A. Usalama barabarani
B. Kulalamika
C. Kukosa magari
D. Hakuna serikali

**32.** Sehemu ya pinde za barabara na milima imetajwa kama? ______
A. Sehemu ya Nakuru
B. Sehemu nzuri ya kuishi
C. Abiria waliolala
D. Sehemu hatari kwa ajali

**33.** Bidhaa za wizi ______
A. huuziwa watu bila wao kujua
B. hununuliwa na wezi
C. huuziwa serikali
D. huuziwa madereva

**34.** Madereva wa Nairobi- Nakuru wamelalamika ______.
A. mara ya kwanza
B. mara moja
C. mara hii
D. zaidi ya mara moja

**35.** Sehemu ipi haikutajwa hapa?
A. Mogotio  B. Nakuru
C. Eldama Ravine  D. Molo

**36.** Vyombo vya habari si kama ______
A. runinga  B. rununu
C. gazeti  D. redio

**37.** Ukosefu wa usalama ni
A. kukosa magari
B. hali nzuri
C. jambo la kufurahia
D. jambo la kuhuzunisha

**38.** Ni nani hushambuliwa mara nyingi?
A. Madereva wenye bidhaa.
B. Watu wa Salgaa.
C. Abiria waliolala.
D. Maafisa wa polisi.

**39.** Inaonekana mwandishi ______
A. labda ni mwizi
B. anajali maisha ya binadamu
C. ni ofisa wa polisi
D. ni dereva

**40.** Kichwa mufti hapa katika habari hii ni ______.
A. Usalama barabarani.
B. Serikali na Salgaa.
C. Wizi wa madereva.
D. Maisha barabarani.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma kifungu kisha ujibu maswali* 41 – 50**

Ilikuwa siku ya Jumatano katika muhula uliopita. Timu yetu ya kandanda ilienda kwenye shule jirani ili wakacheze nao. Timu yetu **iliwasili uwanjani** mwendo wa saa nne alasiri.

Baada ya muda wa nusu saa, timu zote mbili ziliingia uwanjani. Refa wa mechi aliitwa Bwana Kopere. Alipowasili uwanjani alipuliza kipenga chake ndiposa mechi **ikang'oa nanga**.

Timu zote mbili zilipimana nguvu kwelikweli. Kwenye dakika za mwisho katika kipindi cha kwanza, mchezaji wetu anayeitwa Obongo alitoa mkwaju mzuri hadi ndani ya lango. Mabao yakawa moja kwa sufuri. Ikiwa ni fursa yetu na shangwe na mbwembwe kwetu sote. Lo! furaha yetu ilikatika punde tu pale mshambulizi Matata wa timu hiyo nyingine alipofunga bao kwa ustadi. Hatimaye mabao yakawa moja kwa moja.

Mchezo ulipokwisha tulikuwa tumetoshana nguvu.

**41.** Mchezaji aliyefunga bao la kwanza aliitwa ________.
A. refa
B. Obongo
C. Komoro
D. Bwana. Kopere

**42.** Timu yetu ilienda kucheza na timu ya jirani siku gani?
A. Jumatano
B. Ijumaa
C. Alhamisi
D. Jumapili

**43.** Timu yetu ilienda kucheza na timu ________.
A. ya mbali
B. shule ya upili
C. shule mbaya
D. ya shule ilioko karibu na njia

**44.** Mchezo wa kandanda pia huitwaje?
A. wa kiuno
B. wa kabumbu
C. wa mieleka
D. wa kung'ang'ania

**45.** Neno **ikang'oa nanga** limepigiwa mstari. Maana yake ni ________.
A. kuanza safari
B. kuwa chonjo
C. kumakinika
D. kuongeza

**46.** Ni mchezaji gani aliyefunga bao la timu jirani?
A. Kopera
B. Obongo
C. Mchezaji hodari
D. Hatujaelezwa

**47.** Mechi ilipokwisha timu zote mbili zilikuwa ________.
A. bao moja bila jawabu
B. sufuri bin sufuri
C. bao moja kwa moja
D. bao mbili kwa mbili

**48.** Neno "**iliwasili uwanjani**" lina maana gani?
A. ilipatwa
B. ilifika
C. iliweka
D. ilionwa

**49.** Furaha ya timu ya mwandishi ilimalizika wakati gani?
A. Walipofungwa mabao mawili
B. Mchezo ulipokwisha
C. Mchezo ulipoanza
D. Walipofunga bao

**50.** Anayechezesha mpira wa kandanda huitwa aje?
A. Mwalimu
B. Kinara
C. Refa
D. Kiranja